MWONGOZO 25 copies.



# SHULE YA UPILI YA MARANDA

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

MTIHANI WA KITANGUIZI MWIGO 2022

102/2 **KISWAHILI (LUGHA)** Karatasi ya 2

Juni 2021 – Saa: 2½

---

Jina : ....Sylvance.................................................. Nambari yaUsajili: ...............

Mkondo: ........... Sahihi ya mtahiniwa: ................ Tarehe: ......../06/2022.

---

**Maagizo**

*(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*(b) Andika mkondo wa kidato chako kisha tia sahihi yako na uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*(c) Jibu maswali **yote.***

*(d) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

*(e) Majibu yote **sharti** yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

*(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*

***(g) Karatasi hii ina kurasa 9 zilizopigwa chapa.***

***(h) Watahiniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

---

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

CamScanner

a) Ni mambo yepi yalimfanya Mfinyanzi kughairi nia ya kustaafu kwake. (alama 2)

1: Uzalendo / taifa lilimtegemea ② ili kuliendeleza kiuchumi.

2: 2x1 = 2

b) Ni sababu zipi zinadhihirisha wafinyanzi kama wazalendo. (alama 5)

1: Kughairi nia ya kustaafu mapema.

2: Kurauka asubuhi na kutembea masafa marefu kufika shuleni.

3: Kusalia shuleni kuwasaidia wanafunzi baada ya saa za kazi.

4: Kukosa kula staftahi na chamcha.

5: Kukosa kuona familia zao. 5x1 = 5

6.

c) Mfinyanzi ana majukumu gani katika taifa? (alama 2)

1: Kuwashauri wanafunzi.

2: Kuandaa kesho ya wanafunzi / kuwafunza. 2x1 = 2

d) Wanaorejelewa kama udongo wana matatizo kielimu. Thibitisha. (alama 4)

1: Wanaichezea kesho yao.

2: Walimu wanabaki shuleni kuwasaidia kina Sufuri.

3: Kughairi ushauri kama kiburi.

2x2 = 4

e) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika kifunguni: (alama 2)

i. Utuvu Utulivu / pumziko 1x1 = 1

ii. Kunishika sikio Kunishauri 1x1 = 1

Sarufi – itegemee alama

Hijai 6x½ = 3

5

a) **Fupisha aya ya kwanza na ya pili. (maneno 60)** **(alama 9)**

Matayarisho.

**Jibu.**

- ☑ *Mtihani ni kigezo cha kupima werevu wa mwanafunzi.*
- ☑ *Njia hii imetumiwa miaka mingi kukadiria uwezo wa mtu.*
- ☑ *Kuna wanaopinga*
- ☑ *Wanasema mtihani hupima ukadirifu wa mambo kikasuku.*
- ☑ *Huwa na vitisho na shinikizo.*
- ☑ *Mtihani huwapa wanafunzi wasiwasi.*
- ☑ *Ndicho kigezo cha kukadiria kufaulu au kutofaulu.*
- ☑ *Mustakabali wa mwanafunzi kuamuliwa na mtihani.*
- ☑ *Watahiniwa hawajali mengine yanaweza kuathiri matokeo.*

b) **Fupisha aya ya tatu na ya nne. (maneno 50)** **(alama6)**

Matayarisho.

**Jibu.**

- ☑ *Elimu nzuri hufundisha mwanafunzi kutumia akili.*
- ☑ *Mfumo wa kupendelea mitihani haufanyi hivyo.*
- ☑ *Husisitiza yale yaliyoko kwenye mwongozo au silibasi.*
- ☑ *Haupatii mwanafunzi motisha.*
- ☑ *Mwalimu hana uhuru wa kufundisha, anafunza mbinu za kujibu maswali.*
- ☑ *Watahini ni binadamu na uchoka.*
- ☑ *Mtindo wa kukadiria wanafunzi huendelea na kuboreshwa.*

NAMNA YA KUTUZA

- ✓ Mtiririko (alama 2)
- ✓ Ondoa ½ alama kwa kila kosa la **sarufi** litokeapo mara ya kwanza hadi makosa 10
- ✓ Ondoa ½ alama kwa kila kosa la **hijai** litokeapo mara ya kwanza hadi makosa 6
- ✓ Nakala safi na iandikwe kiujazo/mfululizo



M
9) = 08
5 = 05
ut = 02
15

Scanned with CamScanner

CamScanner

6

## 7. MATUMIZI YA LUGHA – ALAMA 40

a) Dondoa **sauti mwambatano** zilizo kwenye maneno haya na utambue mahali kila moja hutamkwa. (alama 2)

i. ngao

☑ */ng/ -hutamkwa kwenye kaakaa laini*

ii. avya *1 x 2= 2*

☑ */vy/ -mdomo-meno*

b) Andika **kivumishi** chenye silabi za muundo ufuatao. (alama 1)

***Konsonanti +konsonanti, irabu +konsonanti+ irabu***

☑ ***mzuri, mrefu, mdogo, mkali***

c) **Tunga sentensi zifuatazo.** (alama 2)

i. arifu

☑ ***Mtoto analia** (jibu liwe taarifa)*

ii. rai

☑ ***Tafadhali niazime kalamu yako/samahani/niwie radhi(ombi)***

d) Andika **mofimu** katika maneno yafuatayo. (alama 4)

i. Muundo

☑ **Mu**- umoja/ngeli(***U-I, umoja***) –**und**- mzizi – **o**- *unominishaji/ kiishio ( 2/ 0)*

ii. Aliaye

☑ A- *nafsi/ngeli* – **li**- mzizi – **a**- *kiishio/ kauli tenda* –**ye**- *kirejeshi* (2/0)

e) Nomino zifuatazo zimo katika **ngeli** gani? (alama 2)

*i.* Parachichi *LI-YA/LI-*

*ii.* [redacted] [redacted]

f) **Andika sentensi ifuatayo katika hali ya wingi.** (alama 1)

Ndoo aliyoivunja shambani mwake ilimkasirisha mtume.

☑ ***Ndoo walizozivunja mashambani mwao ziliwakasirisha mitume.*** **1/0**

g) Onyesha aina za **nomino** katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Biwi la takataka lilizua harufu iliyokasirisha ~~watalii~~. Upendo

biwi la takataka

☑ *biwi –jamii/ makundi,* [redacted] Upendo – Nomino ya Pekee

☑ ***harufu**- dhahania,* [redacted] ***1 x 3=3 (zozote tatu)***

h) Tunga sentensi ukitumia [redacted] **cha 'a' unganifu** chenye dhana ya **aina** au **sampuli .** (alama 1)

Kiwakilishi

☑ *Kitambaa **cha pamba** kimeshonwa vizuri.* ***1 X1 =1***

☑ *Kalamu **ya wino** inaandika vizuri.*

☑ *Nyumba **ya matofali** inapendeza.* ***Sharti apige mstari H+N***



[redacted]

Scanned with CamScanner

CS CamScanner

7

i) Eleza tofauti kisarufi ya maneno yaliyopigiwa mistari. (alama 2)

i. Duka la mwalimu limechomeka.

☑ ***Kivumishi cha 'a' unganifu / RH (Kirai husishi)*** 1x1=1

ii. Duka la mwalimu limechomeka. 1x1=1

☑ ***Kihusishi cha 'a' unganifu***

j) Tunga sentensi kubainisha **kiunganishi cha wakati.** (alama 1)

☑ Atumie **'halafu, kabla ya, baada ya'**

Mwalimu alitufunza virai **halafu** akaondoka. **(1x 1=1**

k) Mwalimu aliingia darasani. Somo lilianza. (alama 1)
(Unganisha kuwa sentensi moja kwa kutumia neno **'pindi'**)

☑ **Pindi** mwalimu alipoingia darasani, somo lilianza. **Au**

☑ Somo lilianza **pindi** mwalimu alipoingia darasani. **1 x 1=1**

l) Bainisha matumizi ya **'na'** katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Nasi tutafunzwa **na** mwalimu yule mgeni.

☑ ***Ufupisho wa nafsi***

☑ ***Kihusishi cha mtenda.***

**1 x 1=1**

m) Tunga sentensi kuonyesha **wakati ujao** hali ya [redacted]. timilifu (alama 1)

☑ **Mwalimu atakuwa** [redacted] amesoma.

☑ [redacted].

n) Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya **ukubwa.** (alama 1)
Mbwa wale wana midomo mikubwa inayotisha

☑ ***Majibwa yale yana madomo makubwa yanayotisha.***

o) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia maneno yaliyopigwa mstari. (alama 1)

Njenga alifunga mlango na kujibu maswali kwa ukakamavu.

☑ Njenga **alifungua** mlango na kujibu maswali kwa ***wasiwasi/woga/ hofu/shauku/ shaka/kiwewe***

***½ x 2=1***

p) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya vitate vifuatavyo. (alama 1)
**Sabuni** na **zabuni**

*(sabuni- kifaa cha kuoshea, zabuni –kandarasi)*

☑ ***Kampuni ya kutengeneza sabuni ya kuoshea nguo ilipewa zabuni ya kusambaza kijijini.***

*Tanbihi: Maana **halisi** ijitokeze wazi kwenye sentensi.)*



Scanned with CamScanner
CamScanner

q) Tumia neno **'pongezi'** katika sentensi kama: (alama 2)

i. Nomino

☑ *Pongezi zake zilipokelewa kwa furaha*

ii. Kihisishi

☑ *Pongezi! Umefuzu vizuri.*

1 x2=2

r) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 2)

KN(W+RH)+KT (t+E)

☑ *Kile cha mwalimu kilikuwa shuleni.*

☑ *Yule wa Onyango atakuwa shuleni.*

☑ *Wale chini ya mti wanapanga njama ya kumpora.* (½ x 4=2)

s) Riwaya hiyo ilikuwa ndefu sana. Wanafunzi waliisoma kwa muda mfupi. (alama 2)

(Unganisha kuunda sentensi changamano)

☑ *Ingawa riwaya hiyo ilikuwa ndefu, wanafunzi waliisoma kwa muda mfupi.*

☑ *Ijapokuwa riwaya hiyo ilikuwa ndefu, wanafunzi waliisoma kwa muda mfupi.*


☑ *Riwaya iliyokuwa ndefu ilisomwa kwa muda mfupi na wanafunzi.*

☑ *Wanafunzi waliisoma riwaya iliyokuwa ndefu kwa muda mfupi.*

... alama 2

t) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi (alama 5)

Wadudu wengine huwasumbua wakulima




½ x 6=3

u) Iandike upya sentensi ukianza kwa **yambwa tendwa.** (alama 2)

Wafula alimkatia nyasi ng'ombe wake kwa upanga.

☑ **Nyasi** zilikatiwa ng'ombe wake na Wafula kwa upanga.

Sarufi - Itegemee alama

HiJai 6×½ = 3



Scanned with CamScanner
CamScanner

**4. ISIMUJAMII (Alama 10)**

***a) Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.***

MHUSIKA 1: Order! Order! Nidhamu, Mheshimiwa Fujo. Hili ni onyo dhidi ya tabia hiyo.

MHUSIKA II: Nisamehe Bwana ………

MHUSIKA I: Sasa ninakaribisha swali la tatu. Mheshimiwa Pekua, uliza swali lako.

MHUSIKA III: Ninaomba kufahamishwa ni kwa nini Waziri wa Maji ameshindwa kusambaza huduma za maji katika kijiji cha Majikame.

I. Bainisha sajili ya makala haya. (alama 1)

Sajili ya bungeni 1x1 =

II. Fafanua sifa za sajili hii kama zinavyobainika kifunguni. (alama 5)

1. Lugha ya bungeni: Mheshimiwa, nidhamu.
2. Lugha mseto/kuchanganya ndimi: Order! Order! Nidhamu
3. Lugha ya heshima: Mheshimiwa, ninaomba.
4. Lugha amrishi: Hili ni onyo dhidi ya…
5. Kukatiza ndimi/kauli: Nisamehe Bwana…
6. Lugha dadisi: Mheshimiwa Pekua, uliza swali lako
7. Lugha elezi/fafanuzi: Hili ni onyo dhidi ya tabia hiyo.

Zozote 5x1

b) Bainisha sababu **nne** zilizopelekea kusanifisha lugha ya Kiswahili. (alama 4)

1. Wingi wa lahaja za Kiswahili.
2. Haja ya kurahisisha mawasiliano.
3. Uvumbuzi wa siasa na teknolojia
4. Haja ya kusawazisha tafiti katika Kiswahili
5. Sababu za kielimu - lugha sawazishi ya kufundishia.
6. Sababu za kidini - lugha sawazishi ya mahubiri.

Za kwanza 4x1 =

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**

Sarufi $4 \times \frac{1}{2} = 2$

Hijai $4 \times \frac{1}{2} = 2$

CS CamScanner